

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

SHULE YA SEKONDARI NGUVUMOJA,  
S.L.P 6,  
**IGUNGA.**  
08/12/2020.

Kumb.Na. NGVSS/J1/15/2021/01

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....

SHULE YA MSINGI ATOKAYO.....

S.L.P 4,

**IGUNGA.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI NGUVUMOJA-2021**

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kidato cha kwanza katika shule yetu mwaka 2021. Shule ipo Km 21 kusini mwa makao makuu ya wilaya Igunga, Mkoa wa Tabora.

Masomo katika muhula wa kwanza yataanza tarehe 11/1/2021. Unapaswa kuletwa shuleni na mzazi/mlezi ili kusajiliwa siku hiyo kuanzia saa 1:00 asubuhi.

Unahimizwa kumshonea mwanao sare za shule na michezo kwa idadi kama ifuatavyo:

**(A) Sare za shule:-**

1. Wavulana suruali 2- Damu ya mzee, mashati meupe 2 aina ya tetroni mikono mifupi
2. Wasichana sketi 2- Damu ya mzee, mashati meupe 2 aina ya tetroni mikono mifupi
3. Wavulana na wasichana-viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi jozi 2, soksi nyeupe jozi 2

NB: Sketi ziwe za kitambaa zenye marinda makubwa ndefu chini ya magoti, suruali kwa wavulana zenye marinda (celebration) na mkanda mweusi wa kuvaliwa kiunoni.

4. Wavulana na wasichana – Tai ndefu rangi ya damu ya mzee
5. Sweta 1 rangi ya damu ya mzee-ili kujikinga na baridi

**B. Sare za michezo**

- (i) **Wavulana** – Bukta 1 nyekundu, fulana 1 nyekundu
- (ii) **Wasichana** – Track suti nyekundu  
-Raba jozi 1 kwa wote

**C. Vifaa vya darasani**

- Daftari 9 aina ya counter book quire 3, kalamu ya wino blue/black, Mkebe 1 wa Hisabati.

**D. Maagizo kwa Mzazi**

- i. Apimwe afya na kuleta Medical Examination Report
- ii. Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi watajaza mkataba kufuata sheria za shule na maagizo ya serikali yatakayotolewa
- iii. Kama mwanafunzi hataletwa shuleni zaidi ya wiki mbili (2) baada ya shule kufunguliwa mzazi /mlezi ataripotiwa kwa Afisa mtendaji wa kata kwa hatua zaidi.

***Mzazi: Kumbuka kula chakula kwa mtoto mchana akiwa shuleni inaweza saidia kuboresha maendeleo ya ufaulu mzuri kwa mtoto wako na kwa shule yetu kwa ujumla. Utapewa mahitaji ya mchango wa chakula utakapofika shuleni.***

**E. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria za ELimu hapa nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia sheria na kanuni za shule.

- a) Heshima kwa viongozi ,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
- b) Mahudhurio mazuri shuleni katika kila shughuli za ndani na nje ya shule
- c) Kufahamu na kuheshimu mikakati ya shule.
- d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- f) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

**F. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE**

- i. Wizi
- ii. Uasherati na ushoga
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama bangi, kokeni, mirungi ,kuberi n.k
- v. Kupiga au kupigana
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- vii. Kudharau Bendera ya Taifa
- viii. Kuoa au kuolewa
- ix. Kupata Mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
- x. Kugoma ,kuchochea na kuongoza au kuvunja amani na usalama wa shule au watu
- xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

**G. KIAPO CHA KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE**

Mimi.....mbele ya mzazi/mlezi wangu.....  
Nimekubaliana na Masharti yote niliyoelekezwa na naahidi kuyatekeleza.

.....  
Saini ya mzazi

.....  
saini ya mwanafunzi

***Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na uyatekeleze kikamilifu***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....  
**PETER CHARLES KINYASI**  
**MKUU WA SHULE**

**MAWASILIANO:- M/SHULE      0786852556**